# Learning by Ear – Religious Dialogue: "A Bridge over Gori"

# Episode 08: "Kumpata rafiki,kumpoteza rafiki"

**Author: Romie Singh**

**Editors: Katrin Ogunsade, Naïma Guira**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Expert on African religions: Jean-Félix Belinga Belinga**

**KISUAHELI ERIC PONDA/THELMA MWADZAYA**

**List of characters for episode 8:**

- Narrator /Philip, male (17)
- Sister Rebecca, female (28)
- Hassan, male (12)
- Father Barnabus (Harry's Uncle) male (49)
- Harry, male (17)
- Layla, female (16)
- Roshi, female (16)
- Mat, male (17)
- Marian Okru, female (16)
- + Patients murmuring in hospital background
- + Students chatting in background -indoors

1. **<u>SIG TUNE UP</u>**

2. **<u>INTRO:</u>**

**Hujambo na karibu kwa sehemu ya nane kwenye mfululizo huu wa vipindi vya NOA BONGO-JENGA MAISHA YAKO, ya mchezo wa Redio "Daraja la Gori".Hii ni hadithi ya kusisimua inayoelezea jinsi Dini na siasa zinavyoweza kutumiwa kusababisha uhasama baina ya jamii mbili na Familia mbili za mji wa Gori…. Kadhalika vijana wawili wanaolazimika kulificha penzi lao. Katika kipindi cha leo, utasikia jinsi Hassan alivyobadilika na kuwa mpya na iwapo Harry atanasa kwenye mtego wa Philip. Philip ni rafiki wa kweli wa Harry ila naye pia ana hisia na Layla.Yeye ndiye msimulizi wa kisa chote.Tega sikio!**

**3.** PHILIP/NARRATOR: Kisa cha usiku ambapo Hassan, mdogo wake Layla alipojaribu kuliteketeza kanisa katoliki mjini Gori, kiliyachagiza makundi ya kijamii kuziimarisha harakati zao za kuutanzua mzozo baina ya Jamii za Waislamu na Wakristo. Lakini sikuyatia shughuli hayo.Nilikuwa na lengo moja tu,la kumshawishi Layla. Wakati huo huo Hassan aliendelea kupata nafuu

Hospitalini ambako Muguuzi Rebecca, aliye na roho ya dhahabu alifanikiwa kumbadili mtazamo.

**Scene 1. In hospital**

**Hassan, Sister Rebecca**

**4. SFX: Door opening, steps coming in, other patients murmuring in the background**

**5. SISTER REBECCA:** **Habari Hassan. Unajisikiaje sasa? Nimekuletea chakula…kiamsha kinywa.!**.

**6. SFX: dishes clattering, tray being placed on a table**

**7. HASSAN:** **Habari Rebecca. Leo najisikia vizuri zaidi..ummm.. nikuulize Swali kuhusu dini yako?**

**8. SISTER REBECCA:** **Sawa!**

**9. HASSAN:** **Jana uliniambia munajiita Walemba**?

10. **SISTER REBECCA:** **Haswaa.. Miaka elfu mbili mia saba iliyopita, kulikuwa na makabila kumi katika ufalme wa Israel ,ambayo yalilazimika kwenda uhamishoni.Waliishi katika maeneo yanayojulikana hivi sasa kama Iraq na Syria. Kisha baadaye makabila hayo yalisambaa kote kusini kupitia Ethiopia. Ntakuonyesha kwenye hii ramani niliyokuletea..!.**

11. SFX: rustle of paper

12. **HASSAN:** **Je walisafiri hadi Afrika Mashariki?**

13. **SISTER REBECCA:** **Tunadhani hivyo.. Hebu tazama hii picha ya magofu nchini Zimbabwe. Sisi Walemba tunaamini kwamba Mababu zetu ndio walioujenga mji huu wa zamani.Lakini pia kuna Wayahudi wengi sana katika sehemu zote za Afria Mashariki na Magharibi.**

14. **HASSAN:** **Hmm. Hilo limeandikwa hapa.**

15. SFX: rustle of paper

16. **HASSAN:** **Ulisema Walemba wana utamaduni wa *kisemiti* –una maana ipi?**

17. **SISTER REBECCA: Semiti ina maana Myahudi. Lakini Wayahudi na Waislamu wanatokea kwenye chimbuko moja. Wote ni kizazi cha Abraham, ingawaje Wayahudi wanaiita Judaea au Israel, na Waislamu nao kwa Arabuni wanasema Mecca na Madina.Kuna baadhi ya tamaduni ambazo zinafana kati ya jamii hizo mbili kwa mfano munasema nyama ni Halal nasi twasema ni Kosher.Maana yake ni ile ile-kwamba mnyama yule amechinjwa kwa jina la Mwenyezi Mungu.Sisi wa kabila la Lemba tunachinja kwa njia hiyohiyo.Nyie hamli nguruwe nasi pia ni hivyo.Sasa waona hakuna tofauti enhe?**

18. **HASSAN: Dada Rebecca?**

19. **SISTER REBECCA:** Bee **Hassan.**

20. **HASSAN:** Nitakaporejea nyumbani **utakuja kunitembelea?**

21. **SISTER REBECCA: (warmly) Hassan, Ningependa sana kufanya hivyo. Tutamuuliza babako na akiridhia ntakuwa nikija kukuchukua wikendi tukatembee pamoja na binti yangu.**

**22. HASSAN:** **Anaitwa nani?**

**23. SISTER REBECCA:** **Abigail. Mwaka ujao atatimiza miaka 10.**

**24. HASSAN:** **Kwa hivyo naweza kwenda nyumbani Kesho? Tafadhali!**

**25. SISTER REBECCA:** ***(laughing)*** **Bila shaka. Majeraha yako ya moto sasa yanaendelea kupona! Umepata nafuu haraka sana kijana wangu!! Sasa maliza chakula chako!**

**26. <u>SFX: dishes clattering</u>**

**27. <u>BRIDGING MUSIC</u>**

**28. PHILIP/NARRATOR:** **Hassan hakuufahamu uzito wa mambo yaliyokuwa yakimsubiri. Kasisi Barnabus alikuwa amewasilisha kesi dhidi yake katika kituo cha Polisi cha Gori kufuatia jaribio la kuteketeza kanisa lake. Hassan hakujua hilo..!.Lakini Harry alifahamu yote na ndio sababu akamwendea Babake mdogo kumrai.Walikaa wote kitako kanisani.**

**<u>Scene 2. In a church (echo on voices)</u>**

**Father Barnabus, Harry**

**29. <u>SFX: church bells ringing 5 o'clock</u>**

**30. FATHER BARNABUS: Kijana yule mpumbavu!Badala ya kuliteketeza kanisa alijichoma mikono!**

**31. HARRY: Huyu kijana ana miaka 12 tu Baba mdogo. Alifiliwa na mamake miezi michache iliyopita.Yuko katika wakati mgumu na amejazwa fikra mbaya tu.**

**32. FATHER B: Kwanini unamtetea? Oooh najua kwanini! Unampenda Dadake Layla. Harry Pole sana ,… nakuonea huruma sana!. Badala ya kuyatilia maanani mandalizi ya kuwa kasisi baada ya kumaliza shule,unapoteza wakati wako ukiwatetea makafiri!**

**33. HARRY: Kama wao ni makafiri na sisi pia ni makafiri. Argh! Sasa ya nini kuitana majina. Baba mdogo, tafadhali,- nakiri Hassan alikosa. Lakini upendo na imani yako ya Kikristo na hata busara za uongozi wako katika jamii ya Ubuntu ziko wapi hapo? ….Ubinadamu wako?**

**34. FATHER B:** **Siasa zina mchango wake hapa.Hili si suala la Hassan tu. Azma hasa ni kuhakikisha kuwa Baraza la Waislamu halipati nafasi ya kuujenga msikiti katika ardhi hiyo iliyo na thamani kubwa!Sisi pia tunaing'ang'ania ili tujenge kanisa kuu la dayosisi.Shambulio hili kwa kweli limenipa nafasi nzuri na wengi wananiunga mkono.Hata Mhubiri Henry Immanuel wa kanisa la Imani moja ameahidi kutoa mchango wa dola elfu 10 za Marekani.Kwasababu ya hilo tuna uhakika wa kupata wingi wa kura katika Baraza la Maendeleo.**

**35. HARRY:** **Ungependa kushirikiana na huyo anayeitwa Mchungaji! Huyo mtu ni laghai! Anawaibia waumini maskini!**

**36. FATHER B:** **Harry,fuata shughuli zako za kuwa kiranja wa chuo haya mengine niachie mimi.**

**37. SFX: Church bells ring**

**38. FATHER B:** **Wakati wa sala ya jioni umefika.Waonaje ukijiunga nasi kwenye maombi kwa leo?**

**39. HARRY:** ***(softly)*** **Basi nitakuombea ubadilike Baba mdogo**!

**40. <u>BRIDGING MUSIC</u>**

**41. PHILIP/NARRATOR:Hatimaye, Harry alikuwa na furaha chuoni. .Layla amerejea baada ya mdogo wake Hassan kuondoka Hospitalini na Babake Ishmail Omer ndiye anayemtazama akiwa nyumbani.Ni siku ya Alhamisi,kwahivyo Mimi, Layla, Harry na Marian tutakutana katika ukumbi wa Mjadala na Mdahalo ifikapo saa tisa alasiri.Muda wa kuutimiza mpango wangu ulikuwa umefika!Ninapoyakumbuka yaliyotokea awali naona kama nilikuwa nilishikwa na wazimu kwa muda.**

**<u>Scene 3. At the Debating club</u>**

**Layla, Harry, Mat, Roshi, Marian, students**

**42. <u>SFX: Background chat</u>**

**43. LAYLA:** **Namshukuru sana Marian kwa kuyakaimu majukumu yangu wakati nilipokuwa na udhuru.Nawashukuru nyote pia kwa kufika hapa.Mjadala wa leo ni: Kwanini wasichana hawapendi kufayna masomo ya Hesabu na Sayansi? Naam ... Roshi ?**

**44. ROSHI:** **Ningetaka sana kulifanya somo hilo lakini, kila nikijaribu naona ni kama lugha tofauti nisiyoielewa.Labda ni kwasababu ya mbinu zinazotumiwa kutufunza.**

**45. MAT:** Inategemea pia na **mazingira ya kijamii. Katika mataifa ya China na Urusi wanawake wanahimizwa kusoma Sayansi na Hesabu**.

**46. MARIAN:** **Ni kweli kabisa , Matt – hilo linatokea katika Mataifa ambayo imani zisizomtambua Mwenyezi Mungu ndizo zinazopewa uzito mkubwa.**

**47. <u>General murmur among the students some agree; some don't</u>**

**48. MARIAN:** **Naamini somo la sayansi ni hatari kwasababu linayapinga mafunzo ya Biblia**!

**49. MAT:** **Si kwasababu hiyo, Marian. Sayansi ni elimu. Mwanasayansi ni mtafiti anayetaka kuelezea mambo yanayomzunguka.**

**50. MARIAN:** **Mungu yuko kila mahali. Na hilo ndilo jawabu sahihi . Mwanadamu alivumbua sayansi ili kuwapotosha wanadamu na kuwasogeza mbali na Mungu.**

**51. HARRY:** **Nataka kuwakumbusha tu kwamba Charles Darwin, mwanasayansi wa Uingereza, ambaye anaaminika kuwa na imani potofu alikuwa mfuasi wa kanisa wakati wa ujana wake.Mbali ya hilo alikuwa mdadisi, na mchunguzi wa mambo.Alisafiri sana na akajionea viumbe vingi tofautitofauti na akataka kuijua asili yake.Labda unaweza kusema Mwenyezi Mungu alimshawishi kutafuta majibu ya maswali haya yote na baada ya hapo akaandika kitabu kinachoelezea Chanzo cha Viumbe yaani *Origin of Species.* .**

**52. <u>General murmur among the students some agree; some don't (fade out)</u>**

**53. PHILIP/NARRATOR: Wakati mabishano yakiendelea,niliudondosha sakafuni taratibu mkufu ule uliokuwa na msalaba , kati ya Harry na Layla-ule nilioutoa kwa Harry aliyepewa na Marian kanisani.Mjadala ndio ulikuwa umekamilika tu.Nilitaraji kwamba Layla atauona mkufu huo. Na kweli akauona!**

**<u>Scene 4. In school</u>**

**Layla, Philip, Harry**

**54. <u>SFX: Students talking, leaving the room. Layla picks up a chain from the floor</u>**

**55. LAYLA:** **Hiki ni kitu gani**?

**56. PHILIP:** **Mkufu wa dhahabu wenye msalaba! Ni wako Harry?**

**57. HARRY:** **Aka!? Oooh? Umm...**

**58. LAYLA:** **Harry? Mkufu huu ni wako? Ulipewa na Babako mdogo?**

**59. HARRY:** ***(hesitating)*** **Um..la hasha..um... .. um – nilipewa na Marian kwa kweli.**

**60. LAYLA:** **Marian? Harry? Kwanini? Na kwanini unauvaa? Unajua haturuhusiwi kuvaa vitu vyovyote vinavyoshiria dini yoyote ile hapa chuoni.**

**61. HARRY:** **Sikuwa nimeuvaa….. Sijui ilikuaje hata ukafika sakafuni. Mimi…...**

**62. LAYLA:** **(angry) Hah! Kumbe. Nimechelewa nataka kwenda nyumbani. Tuonane kesho..!.**

**63. <u>SFX: fast steps leaving , door slamming.</u>**

**64. PHILIP/NARRATOR: Harry alikuwa na nafasi nzuri sana ya kusema uongo, lakini hakutana maana ni muaminifu.Jambo hilo lilimshtua sana Layla. Na hapo nikapata nafasi ya kuingilia kati ,kwani niliuona mwanya wa kulitimiza langu!**

65. **<u>SFX: Opening door, fast steps – Philip catches up with Layla</u>**

66. **PHILIP:** ***(whispers)*** **Layla,jee naweza kukusindikiza?**

67. **LAYLA:** ***(louder for Harry to hear)*** **Sawa Philip…. Nitafurahi sana. Tafadhali nisindikize.**

68. **PHILIP/NARRATOR: Nilidhani ningekuwa nimejawa na furaha ila kila hatua niliyoichukua pembeni mwa Layla nilizidi kujilaumu.Nilimuaga tulipofika kwao na nikakimbia mbio kuelekea kwetu.Nilihuzunika sana.Punde si punde picha moja iliyokuwa juu ya meza ya Baba ilinivutia….picha ya mwanamke-mrembo,aliyevutia na mwana mkononi.Sura yake ilinipa kumbukumbu nyingi na haikunitoka akilini…kwanini?Nilinuwia kumjua.Sikuwa na wa kumuuliza!**

69. **<u>SIG TUNE UP</u>**

## 70. OUTRO:

**Na hadi hapo ndipo tunapofika mwisho wa makala haya ya leo Noa Bongo Jenga maisha yako. Nikitumai utaungana nasi tena kwa sehemu ya Tisa ya mchezo huu 'DARAJA LA GORI', ili uweze kufahamu iwapo Harry na Layla watafaulu kuzishawishi familia zao kuumaliza mvutano wao. Kumbuka iwapo una maoni au ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki, tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!**

**END OF EPISODE 8**